



**KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM  
PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS-MIVUMONI  
DAR ES SALAAM**



---

---

**RATIBA NA HUDUMA JUMA KUU NA SIKUKUU YA PASAKA 2022**

**1.0 JUMANNE 12 APRILI 2022**

Hakutakuwa na Misa wala huduma ya ofisi hapa parokiani. Mapadre watakuwa na Misa ya kubariki Mafuta Matakatifu na kuwekwa Wakfu Krisma katika Kanisa Kuu la Mt. Yosefu kuanzia saa 3.00 asubuhi.

**HUDUMA YA OFISI PAROKIA NA MAFUNDISHO**

Huduma ofisi ya Mapadre haitakuwepo kuanzia tarehe 12 - 23 Aprili 2022. Hata hivyo Paroko atafutwe kwenye dharura.

Mafundisho ya Komunio na Kipaimara yatasimama na kuanza tena tarehe 30 April.

Tuzingatie tangazo hili.

**2.0 ALHAMISI KUU 14 APRILI 2022**

**a) Ibada ya Misa:** Itaanza saa **11.30** jioni

**b) Kuosha miguu:** UWAKA wameandaa kina Baba 12 watakaoshwa miguu wanaombwa kufika kanisani saa 11 Jioni.:

**c) Kuabudu Ekaristi/kukeshwa pamoja na Yesu:** Inaanza mara baada ya Misa kwa makundi mawili tu. Jumuiya za mbali wataanza na kufuatiwa na jumuiya za karibu.

**d) Huduma kanisani:** Itatolewa na **Jumuiya ya Mt. LUKA MWINJILI**

Tuje na Rozari na vitabu vya sala kama Hazina ya Sala na Biblia

**3.0 IJUMAA KUU 15 APRILI 2022**

**a) Njia ya Msalaba:** Itaanza saa **1.00 asubuhi** katika Jumuiya ya Mt. Stefano Shahidi kwa kuzunguka kwenye jumuiya sita kama ifuatavyo:

Kituo cha I- Ndg. Kanisio Mgata (Stefano)

Kituo cha II-Ndg. Mariam Haule (Stefano)

Kituo cha III-Ndg. Enock Matungwa (Stefano)

Kituo cha IV - Ndg. Fred Katema (Petro)

Kituo cha V -Ndg. Herment Munishi (Petro)

Kituo cha VI -Ndg. William Zoe (Petro)

Kituo cha VII- Ndg. Nelson Maswe (Faustina)

Kituo cha VIII - Ndg. John Mbwete (Faustina)

Kituo cha IX- Ndg. Venant Mutashobya (Katarina)

Kituo cha X-Ndg. Hilda Peter (Katarina)

Kituo cha XI- Ndg. Emillian Muungano (Alakok)

Kituo cha XII- Ndg. George Peter (Alakok)

Kituo cha XIII - Ndg. Theresia Kinawiro (Monika)

Kituo cha XIV- Ndg. Clavery Rweyemamu (Monika)

Mwisho - Kanisani

Waumini wote tutakutana Mivumoni Centre saa12.30 asubuhi

Tuje na sadaka na vitabu vyenye njia ya msalaba. Kwaya mtatuongoza kwa nyimbo.

Novena ya Huruma ya Mungu itanza rasmi na itasaliwa mara baada ya Njia ya Msalaba kuelekea Dominika ya Huruma ya Mungu.

**b) Ibada ya Ijumaa Kuu:** Itanza saa **9.00 kamili alasiri** na kufuatia kuabudu Msalaba.

**NB: WAUMINI HATUTABUSU MSALABA BALI TUTAUNAMIA TU.**

**c) Huduma kanisani:** -Itatolewa na Jumuiya ya **Mt. YOSEFU MFANYAKAZI** ambao watabaki mara baada ya njia ya msalaba asubuhi kwa ajili ya usafi kanisani na maandalizi mengine.

#### **4.0 JUMAMOSI KUU/USIKU MTAKATIFU 16 APRILI 2022**

##### **a) Misa**

- Ni saa **4.00** kamili usiku na itanza kwa kubariki moto na kuutayarisha Mshumaa wa Pasaka ikitanguliwa na igizo la vijana saa 3 usiku.
- Mishumaa iliyoandaliwa vizuri kuzuia nta isidondoke sakafuni na kwenye mabENCHI itapatikana kwa shs 500/= katika meza ya mauzo ya vijana na tutaingia kanisani kwa maandamano.

##### **b) Huduma Kanisani**

- Itatolewa na **UWAKA (nje) na VIJANA (ndani)** na kuhakikisha ulinzi upo wa kutosha.
- Jumuiya ya **Mt. MARIA GORETI** watafanya usafi kanisani na maandalizi mengine mchana Jumamosi kwa ajili ya Usiku Mtakatifu/Mkesho.

***NB: Hakuna sala za jumuiya asubuhi wala kusanyiko lolote la ibada tunatafakari Mateso ya Bwana Wetu Yesu Kristo. Tutaendelea na Novena ya Huruma ya Mungu kwenye familia zetu.***

### **5.0 JUMAPILI YA PASAKA 17 APRILI 2022**

**a) Misa ni mbili tu.** Misa ya I ni saa **1.00** asubuhi. Misa ya II saa **3.00** asubuhi. Hakutakuwa na misa ya watoto.

**b) Huduma kanisani:** Itatolewa na Jumuiya ya **Mt. MARIA GORETI**

### **6.0 JUMATATU YA PASAKA 18 APRILI 2022**

**a) Misa** ni moja tu na itanza saa **2.00** kamili asubuhi. Pia kutakuwa na ubatizo wa watoto wadogo. Hivyo wazazi na wasimamizi wa watoto watakaobatizwa wafike Parokiani J3 tarehe 11/04/2022 saa 11.00 jioni kwa ajili ya maandalizi.

**b) Huduma kanisani:** Itatolewa na Jumuiya ya **Mt. MARCELINO**

### **7.0 DOMINIKA YA HURUMA YA MUNGU**

**Huduma kanisani:** Itatolewa na Jumuiya ya **Mt. VERONICA**

#### **MUHIMU:**

- Utulivu, uchaji na nidhamu wakati wote wa Misa na Ibada hizi vizingatiwe; mavazi yawe ya heshima
- Utaratibu wa kuingia na kutoka kanisani na pia utoaji wa sadaka na kukomunika uzingatiwe na jumuiya inayotoa huduma ilisimamie hili
- Tushirikiane kugundua mienendo isiyofaa nje na ndani ya kanisa na kutoa taarifa mapema sehemu husika.
- Viongozi wa H/Walei tushirikiane kwa pamoja kipindi hiki cha Juma Kuu kwa uratibu wa mambo mbalimbali. Pale inapobidi tuwajibike
- Tuendeleo kuomba huruma ya Mungu dhidi ya janga la Corona na tuzingatie maelekezo yote ya Afya.